

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
MUUNGANO NA MAZINGIRA

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA



Tarehe: 14/04/2023

## TAARIFA KWA UMMA

### KUHUSU PICHA JONGEFU (VIDEO) YA GARI YENYE KAVA YA TAIRI LENYE NEMBO YA NEMC (WHEEL COVER) INAYOTEMBEA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII

Kumekuwa na picha jongefu inayoambatana na taarifa za upotoshaji inayotembea kwenye mitandao ya kijamii pamoja na makundi ya WhatsApp ikionesha gari lenye kava ya tairi yenyenembo ya NEMC (Wheel cover) limeegeshwa eneo lisilo rasmi likipatiwa huduma.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linapenda kuutarifu Umma kuwa gari linaloonekana katika picha jongefu haina uhusiano wowote na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Aidha NEMC inatumia njia mbalimbali katika kujitangaza ikiwemo kuandaa na kusambaza kava za matairi (wheel covers) zenyenjembe wa mazingira kwa wadau wake.

Aidha magari yote ya NEMC yana namba za usajili na hufanyiwa matengenezo (service) katika gereji iliyoingia Mkataba wa kisheria wa kutoa huduma husika.

Kwa mantiki hiyo kuonekana kwa gari hilo lenye kava ya tairi lenye nembo ya NEMC haimanishi kuwa gari hilo linamilikiwa na Baraza. Hivyo NEMC inapenda kuwasihii wananchi kupuuzia picha jongefu hiyo (video) hiyo iliyoleta taharuki na kuchafua Taasisi ya Serikali.

Dkt. Samuel Gwamaka

MKURUGENZI MKUU-NEMC